# East African Breweries PLC

## Ilani na Ajenda ya Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa njia ya mtandao utakaofanyika 11 Septemba 2025 kuanzia saa tano asubuhi (11 am)

### KWA WENYEHISA WOTE

ILANI inatolewa hapa kwamba Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka ('AGM') wa 103 wa East African Breweries PLC ('Kampuni') utafanyika kwa njia ya mtandao (kwa kutumia mawasiliano ya kielektroniki) mnamo Alhamisi, 11 Septemba, 2025 saa 11:00 a.m. (tano asubuhi), (saa za Afrika Mashariki (EAT), GMT+3), kutekeleza shughuli zifuatazo: -

**SHUGHULI ZA KAWAIDA:**

1) Kupokea, kutathmini na iwapo itakubalika, kuidhinisha Ripoti ya Kila Mwaka na Taarifa za Kifedha Zilizokaguliwa za mwaka uliokamilika 30 Juni 2025 pamoja na ripoti ya Wakurugenzi na Ripoti za Wakaguzi wa hesabu zilizomo kwenye ripoti hiyo.

2) Mgawo wa Faida

   a) Kuthibitisha Mgawo wa faida wa Muda kwa ajili ya Mwaka wa Kifedha uliokamilika 30 Juni 2025, wa Kshs 2.50 kwa kila hisa ya kawaida, uliolipwa baada ya kutolewa kwa kodi ya zuio au withholding tax, mnamo au karibu na 28 Aprili 2025 kwa wenyehisa waliokuwa wamesajiliwa kufikia kufungwa kwa shughuli za kibiashara mnamo 16 Februari 2025.

   b) Kuidhinisha mgawo wa faida wa mwisho wa Kshs 5.50 kwa kila hisa ya kawaida kwa mwaka wa kifedha uliokamilika 30 Juni 2025, ambao utatozwa kodi ya zuio au withholding tax, kama ilivyopendekezwa na Wakurugenzi. Mgawo huo wa faida utalipwa mnamo au karibu na 28 Oktoba 2025, kwa Wenyehisa watakaokuwa kwenye Sajili ya Wanachama kufikia kufungwa kwa shughuli za kibiashara mnamo 16 Septemba, 2025.

3) Kuchaguliwa kwa Wakurugenzi:

   a) Bw. Leo Breen anastaafu kwa mzunguko kuambatana na Kifungu 117 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.

   b) Bi. Ory Okolloh anastaafu kwa mzunguko kuambatana na Kifungu 117 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.

   c) Bi. Lorna Benton aliteuliwa katika mwaka huo kujaza pengo la muda katika Bodi. Anastaafu kuambatana na Kifungu 116 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.

   d) Bi. Hina Nagarajan aliteuliwa katika mwaka huo kujaza pengo la muda katika Bodi. Anastaafu kuambatana na Kifungu 116 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.

   e) Bw. Andrew Ross aliteuliwa katika mwaka huo kujaza pengo la muda katika Bodi. Anastaafu kuambatana na Kifungu 116 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.

4) Kuambatana na maelezo katika Kifungu 769 cha Sheria ya Kampuni ya mwaka 2015, Sura ya 486 ya Sheria za Kenya, Wakurugenzi wafuatao, ambao ni wanachama wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi wa Hesabu & Usimamizi wa Hatari, wachaguliwe kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati hiyo, kwa kutegemea kuchaguliwa tena kwa Wakurugenzi waliotajwa katika Ajenda nambari 3 hapa juu: Felix Okoboi; Jimmy Mugerwa; Leo Breen; na Ory Okolloh.

5) Kupokea, Kutathmini na iwapo itakubalika, kuidhinisha Ripoti ya Malipo ya Wakurugenzi na malipo yaliyofanywa kwa Wakurugenzi kwa mwaka uliomalizika 30 Juni 2025.

6) Kuwateua tena PricewaterhouseCoopers (PwC) LLP kuhudumu kama Wakaguzi wa Hesabu wa Kampuni kwa mujibu wa Kifungu 721(2) cha Sheria ya Kampuni, 2015, Sura ya 486 ya Sheria za Kenya, na kuipa idhini Bodi kuamua malipo yao kwa mwaka wa kifedha unaofuata.

**SHUGHULI MAALUM**

7) Kutathmini na iwapo itakubalika, kuidhinisha azimio la kawaida lifuatalo kama lilivyopendekezwa na Wakurugenzi: "Kwamba kuambatana na maelezo katika kifungu 8.21 cha Kiambatisho cha Kumi na Tatu cha Kanuni za Masoko ya Mtaji (Kuuzwa kwa Hisa kwa Umma, Kuorodheshwa kwa Hisa Sokoni na Uwekaji bayana wa Taarifa) za Mwaka 2023, sera zifuatazo ziwe, na hapa zinaidhinishwa.

   a) Sera ya Mawasiliano ya EABL;
   b) Sera ya Uwekaji bayana wa Taarifa ya Shirika ya EABL;
   c) Sera ya Utatuzi wa Mizozo na Migogoro ya EABL; na
   d) Sera ya EABL kuhusu Malipo ya Bodi kwa nia ya Kuwavutia na Kuwahifadhi Wanachama wa Bodi.

8) Kutekeleza shughuli nyingine yoyote ile ambayo ilani yake itakuwa imepokelewa ifaavyo.

**KWA AGIZO LA BODI**

**ANGELA NAMWAKIRA**
**KATIBU WA KAMPUNI**

**Tarehe: 20 Agosti 2025**

**MAELEZO KUHUSU MKUTANO MKUU WA KILA MWAKA (,AGM')**

1) East African Breweries PLC ('Kampuni') imeitisha na itaandaa mkutano wake mkuu wa kila mwaka (AGM) mtandaoni kwa njia ya kielektroniki, kuambatana na Sheria za Kuundwa kwa Kampuni.

   Wenyehisa wanafaa kujiandikisha, kwa ajili ya kuhudhuria mkutano huu wa AGM wa mtandaoni, kufikia Jumanne, 9 Septemba 2025 saa tano asubuhi (11:00 a.m.) (saa za Afrika Mashariki (EAT), GMT+3) kama ilivyoelezwa hapa chini.

2) Wenyehisa ambao wangependa kushiriki katika mkutano huu wa AGM wanafaa kujisajili kwa kufanya yafuatayo: -

   a) Kupiga simu ***483*810#** kutoka kwa mtandao wowote wa simu na kufuata maelezo yatakayotolewa; au
   b) Kutuma ombi la kusajiliwa kwa njia ya barua pepe kwa eabl.agm@eabl.com; au
   c) Wenyehisa waliowasilisha anwani za barua pepe watapokea kiunganisho au link cha kujisajili kupitia barua pepe ambacho wanaweza kukitumia kujisajili.

   Ili kukamilisha shughuli hiyo ya kujisajili, wenyehisa watahitajika kuwa na nambari ya kitambulisho/pasipoti waliyoitumia kununua hisa zao na/au nambari ya akaunti ya CDSC.

   Kwa usaidizi, wenyehisa wanafaa kupiga nambari hii ya simu ya msaada: (+254) 709 170 041 kati ya saa mbili asubuhi (8:00 a.m.) na saa kumi na moja jioni (5:00 p.m.) kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa.

   Tafadhali, fahamu kwamba shughuli ya kujiandikisha kuhudhuria AGM itafanyika tu kama ilivyoelezwa hapa juu.

3) Shughuli ya kujisajili kwa ajili ya AGM itaanza mnamo Alhamisi, 21 Agosti 2025 saa tano asubuhi (11:00 a.m.) saa za Afrika Mashariki (GMT+3) na kufungwa Jumanne tarehe 9 Septemba, 2025 saa tano asubuhi (11:00 a.m.) saa za Afrika Mashariki (GMT+3).

4) Kuambatana na Kifungu 180 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, stakabadhi zifuatazo zinaweza kutazamwa kwenye tovuti ya Kampuni katika www.eabl.com:
   (i) nakala ya Ilani hii na Fomu ya uwakilishi;
   (ii) taarifa za kifedha za Kampuni zilizokaguliwa za mwaka uliokamilika 30 Juni 2025.
   (iii) Sera zifuatazo ambazo zitaidhinishwa na Wanachama katika Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka:

   a) Sera ya Mawasiliano ya EABL;
   b) Sera ya Uwekaji bayana wa Taarifa ya Shirika ya EABL;
   c) Sera ya Utatuzi wa Mizozo na Migogoro ya EABL; na
   d) Sera ya EABL kuhusu Malipo ya Bodi kwa nia ya Kuwavutia na Kuwahifadhi Wanachama wa Bodi.

   Ripoti hizi zinaweza pia kupatikana kwa kupiga simu nambari ya USSD iliyotolewa hapa juu na kuchagua kiungo cha Ripoti. Ripoti na ajenda zinaweza pia kupatikana kwenye link au kiunganisho cha kupeperusha mkutano moja kwa moja.

5) Wenyehisa wenye nia ya kuuliza maswali au ufafanuzi kuhusu AGM hii wanaweza kufanya hivyo kwa:
   a) Kutuma maswali yao kwa maandishi kama barua pepe kwa eabl.agm@eabl.com; au
   b) Wenyehisa ambao watakuwa wamejiandikisha kuhudhuria mkutano huu wataweza kuuliza maswali kupitia SMS kwa kupiga simu kwa nambari ya ujumbe (USSD) iliyoorodheshwa hapa juu na kuchagua sehemu ya (uliza Swali) kwenye yale yatakayojitokeza; na
   c) Iwapo hayo hayatawezekana, maswali hayo yakiwa kwa njia ya maandishi na yakiwa na anwani ya barua au anwani ya barua pepe ya kupokelewa majibu yanaweza kufikishwa kwa afisi zilizosajiliwa za Kampuni katika Garden City Business Park, Jumba A, Ghorofa ya 5, Barabara ya Peponi, Ukitokea Barabara ya Ngumba, ukitumia Exit 7 katika Barabara Kuu ya Thika, S.L.P. 30161-00100, Nairobi AU yawasilishwe kwa Image Registrars Limited, Ghorofa ya 5, jumba la Absa Towers (zamani ikiitwa Barclays Plaza), Loita Street, S.L.P. 9287-00100 GPO, Nairobi.

   Wenyehisa ni sharti waandike maelezo kamili kuwahusu (majina kamili, Nambari ya Kitambulisho/Nambari ya Pasipoti/Nambari ya Akaunti ya CDSC) wanapowasilisha maswali yao au maombi ya ufafanuzi.

   Maswali yote na maombi ya ufafanuzi ni sharti yaifikie Kampuni mnamo au kabla ya Jumanne, 9 Septemba 2025 saa tano asubuhi (11:00 am). Baadhi ya maswali yatajibiwa wakati wa AGM.

   Baada ya kupokelewa kwa maswali yote na maombi ya ufafanuzi, Wakurugenzi wa Kampuni watatoa majibu kwa njia ya maandishi kwa maswali hayo yaliyopokelewa, ambayo yatatumwa kwa anwani ya barua au anwani ya barua pepe ya kupokelewa majibu, angalau saa 12 kabla ya kuanza kwa AGM. Maswali yote yaliyopokelewa yatajibiwa kupitia njia iliyotumiwa na mwenyehisa. Hii ina maana ya SMS (kwa watakaotumia USSD), Barua pepe, Barua, au Simu. Maswali yatajibiwa pia wakati wa mkutano wenyewe.

   Orodha kamili ya maswali yaliyopokelewa, yakiwa yamepangwa kwa kufuata mada husika, pamoja na majibu yaliyotolewa, itachapishwa katika tovuti ya Kampuni ndani ya saa 24 baada ya mkutano kumalizika.

6) Kuambatana na Kifungu 298 (1) cha Sheria za Kampuni za 2015, Sura 486 ya Sheria za Kenya, wenyehisa walio na haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika AGM wana haki ya kuteua wawakilishi wa kupiga kura kwa niaba yao.

   Mwakilishi huyo si lazima awe mwanachama wa Kampuni. Iwapo Mwakilishi aliyeteuliwa si Mwenyekiti wa AGM, mwakilishi aliyeteuliwa atahitaji kuwa na simu ya mkononi.

   Fomu ya uwakilishi inapatikana katika tovuti ya Kampuni kwa kufuata link au kiunganisho hiki cha mtandaoni: www.eabl.com. Nakala za karatasi za fomu za uwakilishi zinapatikana pia katika Afisi Kuu za Kampuni zinazopatikana Garden City Business Park, Jumba A, Ghorofa ya 5, Barabara ya Peponi, ukitokea Barabara ya Ngumba, ukitumia Exit 7 katika Barabara Kuu ya Thika, S.L.P. 30161-00100, Nairobi AU kutoka kwa Image Registrars Limited, Ghorofa ya 5, jumba la Absa Towers (zamani ikiitwa Barclays Plaza), Loita Street.

   Fomu ya uwakilishi inafaa kutiwa saini na mwenyehisa aliyemteua mwakilishi au wakili aliyeidhinishwa na mwenyehisa anayewakilishwa kwa njia ya maandishi. Iwapo anayeteua mwakilishi ni kampuni au shirika, fomu ya uteuzi inafaa kupigwa mhuri rasmi wa kampuni au kuidhinishwa na afisa au wakili aliyeidhinishwa kuiwakilisha kampuni au shirika hilo.

   Fomu ya uwakilishi iliyojazwa inafaa kutumwa kwa njia ya barua pepe kwa eabl.agm@eabl.com au ifikishwe kwa Image Registrars, Ghorofa ya 5, jumba la Absa Towers (zamani ikiitwa Barclays Plaza), Loita Street, S.L.P. 9287-00100 GPO, na ifike zaidi ya saa 48 kabla ya wakati wa kufanyika kwa mkutano, sawa na kusema kabla ya Jumanne 9 Septemba, 2025 saa tano asubuhi (11:00 a.m.). Mtu yeyote aliyeteuliwa kuwa mwakilishi anafaa kutuma nambari yake ya simu ya mkononi kwa Kampuni kabla ya Jumanne, 9 Septemba, 2025 saa tano asubuhi (11:00 a.m.) Mwenyehisa ambaye usajili wa mwakilishi wake utakataliwa atafahamishwa kabla ya Jumatano 10 Septemba 2025 kumpa muda wa kushughulikia masuala yatakayoibuka.

7) Matukio ya AGM yatapeperushwa moja kwa moja kupitia kiunganisho (link) ambacho kitatumwa kwa wenyehisa wote watakaokuwa wamejiandikisha kushiriki katika AGM. Wenyehisa na wawakilishi waliojiandikisha watapokea ujumbe mfupi (SMS/USSD) kwenye nambari zao za simu zilizosajiliwa, saa 24 kabla ya AGM kufanyika kuwakumbusha kuhusu AGM. SMS/USSD ya pili itatumwa saa moja kabla ya AGM kufanyika, kuwakumbusha wenyehisa waliojisajili na wawakilishi kwamba AGM itaanza katika muda wa saa moja na ujumbe huo pia utakuwa na link au kiunganisho cha kufuatilia matukio moja kwa moja.

8) Wenyehisa na wawakilishi waliosajiliwa wanaweza kufuatilia matukio ya AGM wakitumia link au kiunganisho cha matangazo ya moja kwa moja na wanaweza pia kupata ajenda za mkutano. Wenyehisa na wawakilishi waliosajiliwa wanaweza kupiga kura wakiombwa kufanya hivyo na Mwenyekiti.

9) Kura itapigwa kwa maazimio yote ambayo yameorodheshwa kwenye ilani.

10) Matokeo ya kura yatachapishwa katika kipindi cha saa 48 baada ya kumalizika kwa AGM, katika magazeti mawili yanayosambazwa kitaifa na katika tovuti ya Kampuni.

11) Ili kuhakikisha wanapokea malipo ya mgawo wa faida ya siku zijazo kwa wakati, Wenyehisa wanaombwa kuwasilisha maelezo yao ya benki na pia kuhakikisha wanabadilisha chaguo lao la malipo kuwa kwa njia ya kielektroniki au kwa njia ya simu. Ili kufanya hivyo, wenyehisa wanaombwa kuweka sawa maelezo yao ya kupokea malipo ya mgawo wa faida kupitia moja ya njia zifuatazo.

   a) Kujaza fomu ya kujumuishwa kwenye njia ya malipo kupitia https://eabl.azurewebsites.net/;
   b) Kutuma barua pepe kwa Image Registrars Limited kupitia eabl@image.co.ke;
   c) Kujiunga kupitia USSD kwa kupiga simu nambari ***483*810#** unapojiandikisha kushiriki Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka (AGM).
   d) Wenyehisa ambao wana akaunti za CDS wanaombwa pia kutoa arifa kuhusu mabadiliko ya anwani zao au kuomba malipo yao ya mgawo wa faida kutolewa kupitia akaunti za benki /MPESA kupitia madalali wao wa hisa au benki ya uwekezaji.
   e) Wenyehisa wenye vyeti wanaombwa kuwasiliana na afisi za Image Registrars Limited, Ghorofa ya 5, jumba la Absa Towers (zamani ikiitwa Barclays Plaza), Loita Street, Nairobi kupitia barua pepe eabl@image.co.ke au nambari ya simu 0709 170000.

12) Wenyehisa wanahimizwa kufuatilia tovuti ya Kampuni www.eabl.com mara kwa mara kwa taarifa na maelezo kuhusiana na AGM. Tafadhali tujulishe kuhusu matatizo au changamoto zozote unazoweza kukumbana nazo kwa utatuzi wa haraka kwa kutumia barua pepe eabl.agm@eabl.com au kwa kutumia nambari yetu ya simu ya msaada ambayo ni (+254) 709 170 000 kati ya saa mbili asubuhi (8:00 a.m.) na kumi na moja jioni (5:00 p.m.) Jumatatu hadi Ijumaa.

13) Afisi za Kampuni huwa zimefunguliwa wakati wa saa za kawaida za kuendesha shughuli za kikazi kila siku ya wiki (isipokuwa Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko Kenya) isipokuwa tu ziwe zimefungwa kwa sababu nyingine za kisheria au halali. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, saa zote zilizorejelewa kwenye ilani hii ni za Afrika Mashariki (GMT+3).

14) Tunatambua na kukushukuru sana kwa kutupatia maelezo na taarifa zako binafsi. Kama sehemu ya ahadi yetu kuhusu uwazi, tunaahidi kukusanya, kushughulikia na kulinda maelezo na taarifa binafsi kuambatana na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Kenya na Sera ya Kulinda Taarifa Binafsi ya Kampuni.

**www.eabl.com**